**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO**

Tarehe: 12/06/2025

# TAARIFA KWA UMMA
# TAHADHARI KUHUSU UWEPO WA FEDHA BANDIA.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro anapenda kuutaarifu umma, hususan wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro, kuhusu uwepo wa fedha bandia zinazozidi kuenea mitaani.

Hali hii inatokana na vitendo vya baadhi ya watu wachache wasio na nia njema kwa Wilaya yetu na Taifa kwa ujumla, ambao wamekuwa wakijihusisha na utengenezaji na usambazaji wa fedha bandia kwa maslahi yao binafsi.

Kwa msingi huo, Mkurugenzi anatoa wito kwa wananchi wote kuchukua tahadhari kubwa kwa kuhakikisha wanakagua fedha wanazopokea au kutoa wakati wa kufanya miamala ya manunuzi na mauzo. Hatua hii ni muhimu ili kuepuka kupokea au kusambaza fedha bandia, hasa katika kipindi hiki ambacho vyombo vya dola vinaendelea kufanya uchunguzi ili kuwabaini na kuwachukulia hatua wale wote wanaohusika na uhalifu huu.

Aidha, Mkurugenzi anawahimiza wananchi kutoa ushirikiano kwa vyombo vya Usalama kwa kutoa taarifa haraka endapo watabaini au kuwa na mashaka juu ya mtu au kundi linalojihusisha na utengenezaji au usambazaji wa fedha bandia katika maeneo yao. Ushirikiano wenu utasaidia kuimarisha ulinzi na Usalama wa kiuchumi katika jamii yetu.

**Imetolewa na;**

**Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali,**

**Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro.**

Jengo la Utawala; S.L.P 1 Loliondo; Arusha; Simu+255272535051; Nukushi +255272535051/2535264
Baruapepe:ded@ngorongorodc.go.tzTovuti: www.ngorongorodc.go.tz